**Kampuni ya Rex Energy yaja na teknolojia mpya ya umeme nafuu**

**Na Mwandishi Wetu**

TAKWIMU zinaonesha kuwa asilimia 36 tu ya Watanzania ndiyo wanaopata umeme huku wale waishio maeneo ya vijijini wakiwa nyuma zaidi.

Kuna changamoto mbalimbali zilizokwamisha watu wa vijijini nchini Tanzania kupata vyanzo vya uhakika vya nishati au teknolojia ya umeme.

Kutokana na sababu hiyo, sehemu kubwa ya watu wa maeneo hayo, hutumia mafuta ya taa na kuni kwa ajili ya kupata nishati ya mwanga.

Matumizi ya vyanzo hivyo vya nishati huzalisha hewa yenye sumu, ambayo huchangia mabadiliko yasiyotakiwa ya tabia nchi na kupelekea utoaji wa moshi ambao unasemekana kusababisha saratani.

Wanawake na watoto ni waathirika wakuu wa saratani inayosababishwa na moshi huo wenye sumu.

Ijapokuwa matumizi ya mifumo ya nishati inayotokana na nguvu ya jua yameongezeka kwa kasi katika maeneo mengi, kuna vikwazo vikubwa vinavyokwamisha nishati hiyo kusambaa vya kiwango cha kutosha.
Watu wengi hawawezi kuhimili bei ya mifumo ya nishati ya jua, au wana wasiwasi kuwa mifumo hiyo itashindwa kufanya kazi au kukosa huduma za uhakika litokeapo tatizo.
Lakini pia, ukosefu wa nishati ni moja ya visababishi vikuu vya umasikini, kutokana na ukubwa wa gharama ya mafuta.

Bidhaa hizi pia kama tulivyoona ni hatari na huharibu afya.
Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa mwaka 2012, ugumu wa kuyafikia maeneo ya vijijini na topografia (mandhari ya nchi) yao unafanya usambazaji wa umeme kupitia mfumo wa gridi kuwa mgumu na hivyo kuondoa manufaa ya kiuchumi.
Katika kile, ambacho kinaweza kuonekana mafanikio mengine katika utekelezaji wa juhudi za serikali za kuhakikisha Watanzania wengi wanapata umeme, Kampuni inayoongoza nchini Tanzania kwa usambazaji wa Teknolojia ya Umeme wa Jua, Rex Energy, imezindua teknolojia mpya ya mfumo wa umeme wa Jua kwa matumizi ya nyumbani ujulikanao 3G+ Solar Home System (SHS), ikiwa ni mara ya kwanza kutua nchini Tanzania.

Rex Energy
Quality Solar Solutions

Akizungumza wakati wa sherehe ya aina yake ya uzinduzi wa teknolojia hiyo katika makao makuu ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam........, Mkurugenzi Mtendaji wa Rex Energy, Francis Kibhisa alisema; “Rex Energy imefanikiwa kuwa mbele katika utoaji wa bidhaa bora zilizo suluhu ya soko la nishati ya jua na kwa kuzindua 3G+SHS leo, nawahakikishia wateja wetu bidhaa bora ya SHS kwa mahitaji yao ya jumla.”

Teknolojia hii imejaribiwa nchini Bangladesh, India na Malaysia na nina uhakika ni suluhisho kwa maeneo yasiyofikiwa na gridi vijijini nchini Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla kwa mpango wa muda wa kati,” alisema.

Teknolojia hiyo mpya iliyoanzishwa kwa kuboresha ile ya SHS itasambazwa kote nchini Tanzania na eneo la Afrika Mashariki.
Teknolojia hiyo imebuniwa na mshirika wa Rex Energy, Kampuni ya Nishati ya Solaric Pvt Ltd yenye makao makuu nchini Bangladesh.
Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo ya Bangladesh alisema: “Kwa uvumbuzi wa 3G+SHS, gharama za SHS zimepunguzwa na kadhalika mahitaji ya kuihudumia kwa kiasi kikubwa na kuifanya bidhaa hiyo kuwa yenye faida kibiashara.”

“Rex Energy iliteuliwa kuwa mshirika wetu kwa sababu ya rekodi yao nzuri katika sekta ya nishati ya umeme wa jua na uwezo wao wa kulifikia soko,” alisema.

Uzinduzi wa 3G+SHS pia unatoa suluhu ya masuala ya kuimudu bei, ambayo yamekwamisha watu wengi walio nje ya umeme wa gridi kunufaika na nishati.
“Tuna mfumo wa malipo, ambao unaruhusu wateja kulipa amana na kiasi kilichosalia kulipwa kipindi cha miezi 12 ili kumsaidia mteja kutobeba mzigo wa kulipa mara moja,” alisema.

“Huu ni mfumo wa lipa kadiri ya unavyotumia (PAYG), ambao mteja anamiliki mfumo wa umeme wa jua baada ya kumaliza kulipa sehemu ya fedha iliyobakia. Bidhaa pia imetengenezwa kwa namna ya kuendana na mahitaji ya makundi tofauti ya jamii za vijijini na hata za mjini kwa vile inakuja kwa ukubwa tofauti linapokuja suala la uwezo wa nishati ukihusisha kuanzia matumizi ya mwanga na kuchaji simu hadi kuwezesha vifaa vya umene kama vile runinga; feni, kompyuta mpakato na kadhalika,” Kibhisa anasema

Makamba Street, Rex Investment Building • Mob: +255 713 607 533
Tel: +255 22 218 0109 • Fax: +255 22 218 1996 • Email: info@rexsolarenergy.com • www.rexsolarenergy.com

Rex Energy
Quality Solar Solutions

Akifafanua kuhusu kufanya uzinduzi huo kwa wakati huu, Mkurugenzi huyo Mkuu wa Rex Energy alisema, “Rex Energy imejitoa kwa ajili ya kusaidia juhudi za serikali za kupeleka umeme katika maeneo magumu kufikika, maeneo yaliyo nje ya gridi na masoko mengine yanayokabiliwa na ukosefu wa usambazaji wa umeme wa uhakika. Uzinduzi haungeweza kuja kwa wakati mzuri kuliko huu sasa.

“Hii ni sehemu nzuri ya kuitikia wito wa Serikali ya Tanzania kupitia Mpango wake Kamambe wa Umeme wa kutoa umeme kwa idadi kubwa ya watu wa vijijini ifikapo mwaka 2030. Rex Energy imepanga kutoa teknolojia ya umeme ya 3G+ SHS kwa kaya karibu milioni 1.5 ifikapo mwaka 2020,” Mkurugenzi huyo alisema.

Mradi huo utashuhudia ajira karibu 2, 500 zikitengenezwa katika mchakato huo, ukinufaisha vijana wa ndani, ambao watapewa mafunzo na Rex Energy kuwa mafundi wa kuweka mfumo wa umeme wa jua na au kutoa huduma za mauzo chini ya usimamizi wa mafundi sanifu wa Rex Energy.

Hali kadhalika mawakala wapya watahusishwa kwa ajili ya usambazaji wa 3G+SHS katika mikoa tofauti ya Tanzania huku ajira zaidi zikitarajiwa kupitia miradi ya wajasiliamali wa ndani waliowezeshwa.

Katika hotuba yake, ………… ambaye alikuwa mgeni rasmi alitoa mwito kwa sekta nyingine binafsi, Taasisi Zisizo za Kiserikali na washirika wa maendeleo kuungana na juhudi za serikali katika utekelezaji wa sera, kwa ajili ya maendeleo jumuishi na endelevu.

“Hii ni kazi yetu sote tukiwa na lengo moja la kutoa nishati ya jua katika jamii za vijijini na kwa kufuata mfano uliooneshwa leo hii na Rex Energy, umasikini katika jamii za vijijini nchini Tanzania utakuwa historia,” alisema.

Hata hivyo, alionya juu ya wimbi la msambao wa bidhaa hafifu na za bei ya chee, akisisitiza kuwa zinatishia uhalali wa mifumo ya umeme wa jua wa majumbani kwa vile wateja kwa idadi kubwa, wanakuwa hawapokei huduma inayoendana na thamani ya fedha yao waliyoivujia jasho.

“Kwa sababu hiyo, kuna umuhimu mkubwa kwa watu wetu kujenga tabia ya kununua bidhaa wanazozifahamu. Bidhaa ya 3G+SHS, ambayo sote tumekusanyika hapa kuizindua leo, inaleta pamoja bidhaa mbili za umeme wa jua, za Solaric (mtengenezaji na msambazaji) na Rex Energy (soko la umeme wa jua na msambazaji nchini Tanzania).”

Makamba Street, Rex Investment Building • Mob: +255 713 607 533
Tel: +255 22 218 0109 • Fax: +255 22 218 1996 • Email: info@rexsolarenergy.com • www.rexsolarenergy.com

Rex Energy
Quality Solar Solutions

"Nina uhakika wateja watapata fursa nzuri ya kupata bidhaa mbili katika mfumo mmoja zilizo suluhisho bora la nishati na hivyo kuongeza maradufu thamani ya fedha yao. Hebu tuwe raia wawajibikaji na watiifu wa sheria zinazoongoza sekta ya umeme mbadala na maadili ya kibiashara. Mfano huo umeoneshwa leo hii na Rex Energy na mshirika wake Solaric," alisema.

END.

Makamba Street, Rex Investment Building • Mob: +255 713 607 533
Tel: +255 22 218 0109 • Fax: +255 22 218 1996 • Email: info@rexsolarenergy.com • www.rexsolarenergy.com